BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Nne – Tarehe 04 Disemba, 2023.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Ikulu:

58. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:

Zanzibar ina wataalamu wabobevu katika fani mbali mbali duniani.

(a) Je, Wizara yako inatumia utaratibu upi kuwatambua wataalamu hao.

(b) Je, Wizara inatumia mikakati gani kuwahamasisha katika kutumia fani zao kwa maslahi ya nchi yao.

(c) Je, nchi gani mpaka sasa ambazo Wazanzibari wanaoishi huko wamehamasika sana kuja kwao kujitolea katika gurudumu la maendeleo.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

20. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tunaipongeza Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kujenga mahanga ya wafanyakazi.

(a) Je, Wizara inatambua changamoto ya mahanga katika kituo cha JKU Ngezi.

(b) Je, ni lini mahanga hayo yatajengwa ili kufanikisha ufanisi wa kazi na hadhi ya wafanyakazi wetu.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

32. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Hassan Mwinyi katika ziara zake za kutembelea mataifa mbali mbali amekuwa akitangaza fursa za

uwekezaji katika sekta tofauti hususan utalii, uvuvi na uchumi wa buluu.

Je, kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), ni yepi matarajio ya ongezeko la wawekezaji katika sekta za Uvuvi, Utalii na Mikutano ya Kitaifa (international conferences) na utalii kwa ujumla baada ya ziara za Mheshimiwa Rais katika mataifa mbali mbali.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

4. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

   Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwa wafanyabiashara ikiwemo wafanyabiashara wa vituo vya mafuta.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

10. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

    Pamoja na juhudi zinazochukuliwa kupunguza changamoto zinazotokea na kuwakumba wanaosafiri kupitia baharini kati ya Unguja na Pemba.

    (a) Je, ni utararatibu upi wa malipo uliowekwa kisheria kwa kila aina ya mizigo inayopakiwa katika vyombo vya usafiri kati ya Unguja na Pemba.

    (b) Kwa kuwa kuna tofauti katika kudai pesa za mzigo wakati wa kuupakia na kuushusha bandarini, je, ni kwa kiwango gani Wizara yako inajiridhisha na uzito au ukubwa wa mzigo katika kudai malipo husika.

    (c) Ni lini Wizara yako itaweka mizani kwa ajili ya kupima mizigo katika bandari ya Wete na Mkoani kwa Pemba na Malindi kwa Unguja ili kuwepo uhalali wa malipo hayo.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

34. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Ni upi mkakati wa Wizara yako wa kufanya tafiti za uvumbuzi wa miamba ya madini hususan madini ya kimkakati ambayo yanaweza kutumika katika sekta mbali mbali za maendeleo ya uchumi wa Zanzibar.

**Wizara ya Ardhi, :**

25. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

    (a) Ni changamoto zipi ambazo zinakwamisha uendelezaji wa mji mpya wa makaazi wa Jumbi/Tunguu.

    (b) Je, Wizara yako ina mkakati gani wa kuuboresha mji huo na miji mengine kama hiyo katika suala zima la kuufanya uwe na mandhari nzuri na ya kuvutia (beautification) ikiwemo suala la kupanda miti ya kivuli.

**Wizara ya Afya:**

7. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Kwa kuwa wafanyakazi wa afya wanakabiliwa na changamoto ya leseni zao kuisha muda wake wa matumizi. Na kwa mujibu wa sheria ni kosa kufanya kazi ya utibabu bila ya leseni.

    (a) Je, ni nani mwenye jukumu la kusimamia upatikanaji wa leseni za wafanyakazi wa afya.

    (b) Je, Wizara yako inatekeleza vipi jukumu lake la kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa afya ili kuwaongezea uwezo na kuufanya utaalamu wao uwende na mabadiliko ya wakati.

    (c) Je, kuna masharti gani kwa mfanyakazi wa afya hasa mtaalamu kupatiwa leseni mpya.

48. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tathmini ya maradhi ya saratani katika visiwa vyetu kwa sasa iko vipi.

49. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, tathmini ya vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua iko vipi.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

41. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Tafiti zinaonesha kwamba wanafunzi wetu wengi hususan wanaohitimu elimu ya juu wanakosa uwezo wa kujiamini, kudadisi, ubunifu na kujitegemea.

(a) Je, ni kwa kiasi gani maboresho mapya ya mitaala yanakuja kuondosha changamoto hizi kwa wahitimu wetu wa elimu za juu.

(b) Ni vipi mitaala hiyo itawawezesha wahitimu kuwa na elimu ya ufundi na ubunifu ili wawe na uwezo wa kuja kulisaidia taifa letu na kujisaidia wao wenyewe.

(c) Je, ni matarajio gani wananchi wawe nayo ili kuona kuwa maboresho ya mitaala ya elimu inakidhi mahitaji ya taifa lao na wao wenyewe.

42. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, ni kwa kiasi gani maboresho ya mitaala mipya ya elimu iliyofanywa hivi karibuni, imewashirikisha walimu ipasavyo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

74. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

    (a) Je, ni bidhaa gani zinazozalishwa na Wajasiriamali Wadogo Wadogo hapa Zanzibar ambazo Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) imefanikiwa kuzipatia vibali kwa kipindi cha miaka miwili ya hivi karibuni.

    (b) Je, ni sababu gani za msingi zinazowafanya Wajasiriamali Wadogo Wadogo kushindwa kukidhi vigezo vya ZBS katika utengenezaji wa bidhaa zao.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya 2018 na Kutunga Sheria ya Uwekezaji Zanzibar na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,**
**04 Disemba, 2023.**

**Raya Issa Msellem**
**KATIBU WA BARAZA.**